Mpango wa Uhamasishaji wa Uwazi na Uwajibikaji Katika Sekta ya Madini

Extractive Industries Transparency Initiative

Kituo cha Sheria na Haki za Bi-nadamu - LHRC

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu [LHRC]
Jengo la Jaji Lugakingira
Kijitonyama – Dar es Salaam
S. L. P. 75254
Simu: +255 22 2773038/48 Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

UTAMBULISHO WA KITUO

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kimekua kwa kasi sambamba na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kituo hiki kinafanya kazi nchi nzima kupitia mipango yake ya huduma za mafunzo kwa jamii na ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina ushawishi wa mabadiliko ya sera, sheria na taratibu mbalimbali katika ngazi ya kitaifa kwa kupata nguvu na uhalali wa kuyatenda hayo kutoka kwa jamii.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Makampuni, sura ya 212 ya sheria za Tanzania kama shirika lisilo la serikali, la ku-

jitolea na lisilo jitafutia faida kwa nia ya kugawana.

Shirika hili liliundwa kutokana na mradi wa haki za binadamu wa Shirika la Mpango wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania [TANLET].
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina makao yake makuu jijini Dar es Salaam na ofisi ndogo mkoani Arusha.

Maono

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye HAKI na USAWA.

Tamko la Lengo Mahsusi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kutafuta faida kwa nia ya kugawana, lisilo na fungamano na chama chochote cha siasa, linalojibidisha kujenga uwezo wa

jamii, kulinda, kutetea na kupigania haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

Maadili ya Shirika

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaamini katika maadili ambayo hutoa mwongozo wa jinsi wanachama wake, bodi ya wakurugenzi, wafanyakazi na wadau wengine wanavyopaswa kuenenda. Maadili hayo ni kama yafuatayo:

- Uadilifu;
- Usawa;
- Uwazi;
- Uwajibikaji;
- Weledi; na
- Kujitoa na Kujitolea.

UTANGULIZI

EITI (Extractive Industries Transparency Initiative) ni Mpango wa Uhamasishaji wa Uwazi na Uwajibikaji Katika Sekta ya Madini, ulitangazwa mara ya kwanza kwenye Mkutano wa Dunia juu ya Maendeleo Endelevu uliofanyika Johannesburg, Afrika ya Kusini mnamo Mwaka 2002 na kuzinduliwa rasmi London Uingereza mwaka 2003. Nchi wanachama wa asasi hii ya kimataifa ya EITI hutakiwa kuweka wazi malipo ya kodi kutoka kampuni za uchimbaji wa madini, gesi asilia na mafuta; na mapato yanayopokelewa Serikalini. Kupitia taarifa hizi za malipo ya kodi na mapato wananchi hushirikishwa katika usimamizi wa rasilimali hizi kwa kujadili na kutoa michango yao ili kuboresha sera na sheria kwa ajili ya kuongeza mapato.

SHUGHULI KUU YA EITI

EITI inasaidia serikali na washikadau wengine kama makampuni, vyama vya ushirika, wawekezaji, vyombo vya habari na wengineo kutoa taarifa, kupitia na kukagua kwa utaratibu, malipo yanayotolewa na makampuni na kiasi kinachopokelewa na mawakala wa serikali. Uwazi huu ndio msingi madhubuti wa usimamizi mzuri wa sekta na utawala bora kwa ujumla

KUANZISHWA KWA EITI

Sababu kubwa ya kuanzishwa EITI ni kuweka kiwango cha dunia na kuhamasisha katika kuinua uwazi na uwajibikaji kwenye malipo na mapato ya nchi tajiri kwenye rasilimali za mafuta, gesi na madini kwa kutaka nchi wanachama kutekeleza mambo yafuatayo:

Makampuni husika kuchapisha kiasi inachoilipa serikali.
Serikali ichapishe kiasi inachopata kutoka kwenye makampuni husika.

Msimamizi huru alinganishe taarifa hizi. Takwimu za mapato na hitilafu zake lazima zichapishwe katika 'ripoti za EITI'.

Mchakato usimamiwe na Kamati ya Wadau Mseto ambayo lazima iwe na wajumbe kutoka serikalini, makampuni husika na asasi za kiraia.

NCHI ZILIZOJIUNGA NA EITI

EITI inaundwa na idadi ya nchi zisizopungua 25 kama ifuatavyo, Albania, Burkina Faso, Azerbaijan, Cameroon, Ivory Coast, Ghana, Iraq, Kazakhstan, Jamhuri ya Kyrgyz, Liberia, Mali, Mauritania, Mongolia, Msumbiji, Niger, Nigeria, Norway, Peru,

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Tanzania, Timor-Leste, Togo, Zambia na Sierra Leone.

KUANZISHWA KWA EITI TANZANIA

Mnamo tarehe 18 Novemba, 2008, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa tamko kwa umma juu ya nia yake ya kujiunga na asasi ya EITI ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa sekta za madini, gesi asilia na mafuta. Katika mkutano wa nne wa EITI wa dunia uliofanyika tarehe 16 Februari, 2009 Doha, Qatar, Bodi ya EITI iliipatia Tanzania uanachama wa awali baada ya kukamilisha taratibu za kujiandikisha.

Utekelezaji wa EITI hapa nchini unasimamiwa na Kamati Tekelezi ambayo imeundwa na wajumbe 16 kutoka asasi za kiraia, kampuni na Serikali. Wajumbe watano kwa kila kikundi. Kamati hiyo huongozwa na mwenyekiti ambaye hatoki katika kundi lolote. Katika utendaji

wa shughuli za kila siku, Kamati inasaidiwa na Sekretarieti. Hivyo kwa Tanzania, mpango huu unajulikana kama TEITI (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative).

SABABU ZA TANZANIA KUJIUNGA NA EITI

Tanzania imejiunga na EITI kwa sababu zifuatazo:

- Kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia kwa kuweka wazi malipo ya kodi kutoka kwenye makampuni ya uziduaji na mapato yaliyopokelewa serikalini;

- Kuongeza ufahamu kwa umma kwa kuchapisha malipo na mapato yatokanayo na madini, mafuta na gesi asilia, hivyo kuongeza ushiriki wao katika usimamizi wa sekta za madini, mafuta na gesi asilia;

- Na pia kuisaidia serikali na wadau kupata taarifa sahihi na kwa wakati za malipo na mapato yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia.

MPANGO WA EITI UNAOTEKELEZWA NA TANZANIA

1. Utekelezaji wa EITI hapa nchini Tanzania unasimamiwa na Kamati tendaji ambayo imeundwa na wajumbe 16 kutoka asasi za kiraia, kampuni na Serikali. Wajumbe watano kwa kila kikundi. Kamati hiyo huongozwa na mwenyekiti ambaye hatoki katika kundi lolote. Katika utendaji wa shughuli za kila siku, Kamati inasaidiwa na Sekretarieti.
2. Hivyo Mpango huu wa EITI unatekelezwa nchini Tanzania chini ya

TEITI, kwa kupitia kamati yake tendaji inawataka makampuni na serikali kuweka malipo wazi; Makampuni yaonyeshe yamelipa kodi kiasi gani na serikali ionyeshe imepokea kiasi gani. Ripoti ya kwanza ya mpango huo wa TEITI hapa nchini Tanzania ilitolewa mnamo Februari 8, 2011 na iliibua utofauti kati ya kile ambacho makampuni yalisema yamelipa na kile serikali ilichokiri kupokea.

http://eiti.org/eiti/history

http://www.ap2000.or.tz/reports/ripoti_ya_EITI.pdf

Muungano baina ya Serikali, Makampuni na Asasi za Kiraia, usaidie maliasili za Taifa zinufaishe wote!

Wasiliana nasi:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Legal and Human Rights Centre [LHRC]
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 22 2773038/48; Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Ofisi ya Arusha
Barabara ya Engira, Kitalu Na. 48
S. L. P. 15243 - Arusha
Simu: +255 27 2544187
Barua Pepe: lhrcarusha@humanrights.or.tz

Kituo cha Msaada wa Sheria
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633 - Dar es Salaam
Simu/Nukushi: +255 22 2761205/6
Barua Pepe: legalaid@humanrights.or.tz